

EEC yaahidi kuipatia u. Msumbiji chakula

29/4
88

MAPUTO, Msumbiji p. 2

JUMUIA ya Uchumi ya Ulaya Magharibi (EEC) juzi iliahidi kuipatia Msumbiji tani 127,000 za misaada wa chakula ikiwa ni kuitikia mwito wa Umoja wa Mataifa wa kutaka Msumbiji isaidiwe kwa mwaka 1988/89.

Ahadhi hiyo imo katika salamu kuto-ka kwa Makamu wa Rais wa jumuiya hiyo, Bw. Lourenco Natali, iliyosoma-wa mjini hapa katika siku ya pili ya mukutano unaozungumzia misaada ya dharura kwa Msumbiji, ambao un-agharimiwa na Umoja wa Mataifa.

Salamu hizo, ambazo zilisomwa na mvakilishi wa EEC nchini Msumbiji,

zilisema jumuiya hiyo imeamua kuipa Msumbiji tani 110,000 za nafaka kwa mwaka 1988.

Jumuiya hiyo pia itatoa tani 4,000 za maharage, tani 2,000 za maftuta ya kupikia na tani 1,000 za sukari, vyote vya thamani ya sh. milioni 2,820.

EEC pia itaipa Msumbiji tani 10,000 kuptitia mashirika yasiyokuwa ya serikali, na ruzuku ya sh. milioni 337.4 itatolewa kuptitia mashirika kama hayo na zitatumika kwa ajili ya mpango ya misaada ya dharura.

Bw. Natali alisema Msumbiji inabidi ipewe misaada zaidi kwa sababu "ingawa tayari inakabiliwa na hali mbaya ya uchumi kutohana na hali ya hewa isiyoridhisha, pia inaendelea kukabiliwa na mashambulio yanayofanywa na vikundi vinavyosaidiwa na mataifa ya nje."

Akihutubia kikao cha ufunguzi cha mukutano huo Jumanne Ilyopita, Rais Joaquim Chissano wa Msumbiji aliushutumu utawala wa Makaburu wa Afrika Kusini kwa kusababisha matatizo yanayoikibili nchi hiyo ambayo yamefanya wananchi wa Msumbiji wapatao milioni 5.9 wahitaji misaada ya chakula.

Habari zinasema Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa linataraja kutenga tani 35,000 za chakula kwa ajili ya Msumbiji katika msimu wa kilimo wa 1988/89.